**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**KURUGENZI YA MAWASILIANO YA RAIS, IKULU**

*Dar es Salaam*
*08 Februari, 2026*

Baruapepe: press@ikulu.go.tz

# TAARIFA KWA UMMA

## RAIS SAMIA AFUNGUA SOKO KUU JIPYA LA KARIAKOO, ATOA MWELEKEO MPYA WA UENDESHAJI NA UWAJIBIKAJI

Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan leo amefungua rasmi Soko Kuu Jipya la Kariakoo, jijini Dar es Salaam, na kusisitiza kuwa mradi huo ni sehemu ya mkakati wa Serikali wa kuimarisha mazingira ya biashara, kuongeza tija ya uchumi na kulinda mitaji ya wafanyabiashara.

Rais Dkt. Samia amesema ujenzi wa soko hilo ni matokeo ya dhamira ya Serikali ya kurejesha Soko la Kariakoo baada soko la awali kuteketea kwa moto mwezi Julai, mwaka 2021, kwa kufanya ukarabati na kujenga soko jipya linalozingatia viwango vya usalama, ubora na mahitaji ya biashara ya kisasa.

Rais Dkt. Samia amehimiza uendeshaji wa soko hilo kuzingatia misingi ya ufanisi, nidhamu na ushindani wa haki, na kuongeza kuwa Kariakoo ni mhimili wa biashara ya kitaifa na kikanda, na kitovu muhimu cha uchumi kinachowaunganisha wazalishaji, wasambazaji, wauzaji na wanunuzi kutoka ndani na nje ya nchi.

Vilevile, ameipongeza Ofisi ya Waziri Mkuu – Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), makandarasi, na wasimamizi waliopo na waliopita kwa utekelezaji wa mradi wenye miundombinu yenye ubora wa hali ya juu, ikiwemo mifumo ya usalama na huduma za kijamii, na kuuelekeza uongozi wa soko kuendelea kuimarisha mazingira rafiki kwa wanawake, wakiwemo wafanyabiashara.

***"Nimefurahishwa na uwepo wa huduma rafiki kwa mama na mtoto, hususan vyumba vya kunyonyeshea. Hatahivyo, natoa rai kwa menejimenti ya soko kutenga eneo maalum la kulelea watoto wa akina mama watakaokuwa wanafanya biashara katika soko hili, "*** alisema Rais Dkt. Samia.



*Ikulu Mawasiliano / ikulu_mawasiliano / ikulu_Tanzania / ikulu Tanzania / ikulumawasilano / Ikulu Tanzania / Ikulu Tanzania*

Katika kuhakikisha uendeshaji wenye tija, Rais Dkt. Samia amesisitiza umuhimu wa mifumo thabiti ya zimamoto, uokoaji na dharura, pamoja na upangaji wa ratiba rasmi za kushusha na kupakia mizigo, sambamba na kupunguza msongamano wa watu na vyombo vya usafiri ili kurahisisha shughuli za biashara na kulinda hadhi ya soko.

Kuhusu usalama na ubora wa bidhaa, Rais Dkt. Samia amezitaka taasisi zinazohusika kusimamia kikamilifu ubora wa huduma na bidhaa kwa viwango vinavyotakiwa, kwa kuzingatia kuwa Soko Kuu la Kariakoo ni soko la hadhi ya kimataifa linalopaswa kuendeshwa kwa misingi ya uaminifu na uwajibikaji.

Rais Dkt. Samia ameielekeza Ofisi ya Waziri Mkuu – Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI) kusimamia mchakato wa upangaji wa maeneo ya biashara kwa misingi ya haki, uwazi na usawa, ili kulinda maslahi ya wafanyabiashara waliokuwepo awali na kuzuia mianya ya upendeleo.

***"Nisingependa kusikia viongozi wanahodhi maeneo na kuyakodisha kwa wengine. Shirika la Masoko ya Kariakoo ndilo likodishe maeneo moja kwa moja kwa wafanyabiashara, kwa uwazi, na mapato na matumizi ya upangishaji yawe wazi kwa wote,"*** alionya Rais Dkt. Samia.

Katika eneo la mapato, Rais Dkt. Samia amesisitiza uwajibikaji na matumizi ya mifumo ya kidijitali katika makusanyo na usimamizi wa kodi, na kuiagiza Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) kushirikiana na mamlaka za Serikali za Mitaa kukusanya mapato kwa uadilifu, huku akiwataka wafanyabiashara kulipa kodi stahiki kwa hiari na kwa wakati.

Akihitimisha, Rais Dkt. Samia amesisitiza kuwa Soko Kuu Jipya la Kariakoo ni uwekezaji wa kimkakati wa Taifa unaopaswa kulindwa, kutunzwa na kusimamiwa kwa ufanisi, ili liendelee kuwa injini ya uchumi na mfano wa masoko ya kisasa barani Afrika.

Hafla ya Ufunguzi wa Soko Kuu Jipya la Kariakoo ilihudhuriwa na viongozi mbalimbali wa kitaifa na Serikali, akiwemo Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. Mwigulu Lameck Nchemba (Mb.), pamoja na Mawaziri, Wakuu wa Mikoa na Wilaya, Wabunge, viongozi waandamizi wa Serikali, viongozi wa vyama vya siasa, vyombo vya ulinzi na usalama, sekta binafsi, wafanyabiashara wa Kariakoo, na wananchi.

**TAARIFA KWA MHARIRI**

Kariakoo ni mhimili muhimu wa uchumi na ukusanyaji wa kodi, ambapo wafanyabiashara wake huhudumiwa na Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) kupitia Kanda ya Kodi Kariakoo, Idara ya Walipakodi wa Kati, Idara ya Walipakodi Wakubwa, na Idara ya Forodha. Aidha, ni kitovu cha usambazaji wa bidhaa kwa mikoa yote ya Tanzania Bara na Zanzibar, hivyo kuathiri moja kwa moja uzalishaji, ajira, na mapato ya serikali.

Takwimu zinaonesha kuwa Kariakoo huchangia mapato ya ndani kwa wastani wa shilingi **bilioni 13** kila mwezi moja kwa moja, na si chini ya shilingi **bilioni 500** kwa njia isiyo ya moja kwa moja kupitia Forodha, Walipakodi wa Kati na Wakubwa, na mifumo ya kodi katika mikoa yote nchini.

Bakari S. Machumu
Mkurugenzi wa Mawasiliano ya Rais, Ikulu